# HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGEA

# TAARIFA YA UTENDAJI NA UWAJIBIKAJI WA HALMASHAURI KWA MWAKA 2016/2017 KATIKA KIKAO CHA BARAZA LA MADIWANI TAREHE 04/08/2017

## 1. UTANGULIZI:

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Halmashauri ya Wilaya ya Songea katika mwaka wa fedha 2016/2017 ili tekeleza malengo na shughuli mbalimbali zilizokuwa zimeainishwa katika mpango na bajeti ya Halmashauri. Pamoja na utekelrzaji wa malengo na shughuli hizo pia ilitekeleza majukumu,maelekezo na maagizo yaliyotolewa na vikao halali vya Halmashauri na kutoka kwa Viongozi mbalimbali wa Chama na Serikali.

.Aidha utekelezaji huu ulifanyika kwa kufuata sheria,taratibu na miongozo mbalimbali iliyokuwa ikitolewa na Serikali. Kwa kutekeleza hayo, Halmashauri iliweza kupata mafanikio mengi yakiwemo utekelezaji wa miradi ya maendeleo,kutatua kero za wananchi na kuweza kuboresha utoaji wa huduma za kijamii na kiuchumi kwa wananchi wake

## 2. MWENENDO WA BAJETI

- **Fedha zilizotengwa katika bajeti.**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri ya Wilaya ya Songea iliidhinishiwa kupokea,kukusanya na kutumia jumla ya Sh. **28,806,257,365** kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za Halmashauri. Kati ya fedha hizo **Sh.16,096,281,000** zilikuwa ni za mishahara, **Sh.1,190,513,901** za matumizi mengineyo, **Sh. 8,014,121,539** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo na **Sh.1,472,142,116** ni fedha za mapato kutokana na vyanzo vya ndani ikiwemo na michango ya wananchi..

- **Kiasi cha fedha zilizopokelewa kutoka Hazina kwa ajili ya matumizi ya kawaida,mishahara na miradi ya maendeleo.**

Katika kipindi cha mwaka 2016/2017, Halmashauri ilipokea **Sh. 18,292,573,433** kutoka Hazina ikiwa **Sh. 12,814,319,000** kwa ajili ya mishahara, **Sh. 780,664,348** kwa ajili ya matumizi ya kawaida (OC) na **Sh. 4,697,590,084** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Mapokezi ya fedha hizi ni sawa na asilimia **64** ya fedha zilizokusudiwa**.**

- **Kiasi cha fedha za matumizi ya kawaida, mishahara na miradi ya maendeleo zilizotumika**

Kwa mwaka huu, Halmashauri ilitumia **Sh. 780,664,348** kwa ajili ya matumizi ya kawaida, mishahara **Sh. 12,814,319,000** na matumizi kwa ajili ya miradi ya maendeleo **Sh. 4,887,385,711.**Matumizi kwa upande wa miradi ya maendeleo ni makubwa kuliko mapato hii inatokana na matumizi ya fedha za bakaa za miradi ya mwaka 2015/2016.

- **Bajeti ya fedha za mapato kutokana na vyanzo vya ndani vya Halmashauri (Own source)**

**Mheshimiwa mwenyekiti**, Katika mwaka 2016/2017 Halmashauri ilikisia kukusanya jumla ya **Sh. 1,472,142,116** kutoka vyanzo vyake vya ndani. Hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha 2016/2017, Halmashauri ilikuwa imekusanya jumla ya **Sh. 938,569,977** toka vyanzo vyake vya ndani ikiwa sawa na asilimia **64**. Halmashauri katika kipindi cha miaka mitano mfululizo iliyopita ilikuwa haijawahi kuvuka nusu ya makusanyo yake kwa vyanzo vya ndani. Kwa mwaka 2016/2017 imevunja rekodi hiyo na hii imetokana kwa kiasi kikubwa na mikakati iliyowekwa na ukusanyaiji wa mapato kwa kutumia mashine za ki –electronic. (POS).

**JEDWALI NA. 1 LINAONYESHA MCHANGANUO WA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO ZILIZOPOKELEWA NA KUKUSANYWA KATIKA SEKTA MBALIMBA KWA MWAKA 2016/2017.**

| NA | JINA LA MRADI/SEKTA | FEDHA IDHINISHWA(TSh.) | FEDHA TOLEWA (TSh.) | FEDHA TUMIKA (TSh.) | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | RUZUKU YA MAENDELEO YA KUJENGA MITAJI (LGCDG) | 437,922,000 | 153,134,000 | 153,134,000 | Fedha zimepokelewa miradi inaendelea kutekelezwa |
| 2 | MFUKO WA JIMBO | 40,199,000 | 47,363,000 | 47,363,000 | Fedha zimepokelewa na zinaendelea kutekeleza miradi. |
| 3. | UJENZI WA NYUMBA MAZINGIRA MAGUMU | 400,000,000 | 0 | 0 | Fedha hazijapokelewa. |
| 4 | MPANGO WA MAENDELEO YA ELIMU YA SEKONDARI (MMES) | 447,312,000 | 0 | 142,451,199 | Miradi inaendelea kutekelezwa kwa fedha za bakaa. |
| 5. | ASDP - DADG | 461,685,000 | 0 | 6,300,000 | Shughuli zilifanyika kwa fedha za bakaa. |
| 6. | MRADI WA MIVARF | 42,755,000 | 12,000,000 | 16,826,400 | Usimamizi na ufuatiliaji ulifanyika |
| 7 | MFUKO WA BARABARA (ROAD FUND) | 888,110,000 | 885,091,317 | 421,878,781 | Miradi inaendelea kutekelezwa |
| 8 | MPANGO WA UJENZI WA BARABARA ZA RAMI MAKAO MAKUU | 2,500,000,000 | 0 | 0 | Fedha hazijatolewa. |
| 9 | MPANGO WA KUPAMBANA NA UKIMWI (HIV/AIDS) NMSF | 41,179,539 | 0 | 32,091,954 | Shughuli zilifanyika kwa fedha za bakaa. |
| 10 | MPANGO WA USAMBAZAJI MAJI VIJIJINI NA USAFI WA MAZINGIRA (RWSSP) | 4,996,930,090 | 624,261,517 | 285,930,808 | Kazi zinaendelea kwa kutumia fedha za bakaa |
| 11 | MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASKINI (TASAF III) | 1,408,725,000 | 2,095,903,029 | 2,095,051,260 | Mradi unaendelea |
| 12 | MFUKO WA PAMOJA WA AFYA (HSBF) | 429,914,000 | 429,914,000 | 429,914,000 | Shughuli zinaendelea kutekelezwa. |
| 13 | MCHANGO WA HALMASHAURI KATIKA MIRADI YA MAENDELEO | 748,25,000 | 115,365,000 | 115,365,000 | Miradi inaendelea kutekelezwa |
| 14 | MRADI WA MAJI KIJIJI CHA LIPAYA | 42,020,000 | 42,020,000 | 0 | Fedha bado hazijaanza kutumika |
| | **JUMLA** | **8,014,121,539** | **4,697,590,084** | **4,887,385,711** | |

## 3.0 MALENGO YA KISEKTA NA UTEKELEZAJI WAKE

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Halmashauri ilitekeleza majukumu yake na kupata mafanikio katika Sekta,Idara na Vitengo vyake mbalimbali kama ifuatavyo;

### 3.1 Sekta ya Maji:

Halmashauri iliendelea kutekeleza mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Sekta ya Maji awamu ya pili (WSDP II) ambao ni utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maji inayoelekeza upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi umbali wa mita 400 kutoka katika makazi yao. Wananchi wapatao 84,189 sawa na asilimia 59.22% ya wakazi wote katika Halmashauri wanapata huduma ya maji safi na salama. Visima vya asili na ujenzi wa visima vifupi umechangia sana katika kupunguza kero ya maji katika Halmashauri. Lengo ni kufikia asilimia 85 ya wakazi wote ifikapo mwaka 2025 kama sera ya maji inavyoelekeza.

Kwa mwaka 2016/2017 Halmashauri iliendelea kutekeleza miradi ya maji 5 katika vijiji vya Liula, Lipaya, Maposeni/Namakinga,Muhukuru Lilahi na Mradi wa Luyeleha unaojumisha vijiji vya Lugagara,Muunganozomba, Mdunduwalo,Maposeni,Lundusi,Peramiho A,Peramiho B na Morogoro. Mradi wa maji kutoka katika chanzo cha Namakinga unaoleta maji katika Ofisi za Makao makuu ya Halmashauri hapa katika kijiji cha Lundusi umekamilika na huduma ya maji inapatikana ya kutosha kwa sasa.

Mradi wa maji katika kijiji cha Liula utakamilika ifikapo Agosti 30,2017. Vituo 30 vinatoa maji Mradi wa maji katika kijiji cha Lipaya ujenzi wa intake unakamilishwa na kazi ya kufyatua tofari kwa ajili ya ujenzi wa tanki unaendelea.Mradi wa maji wa Luyeleha mkataba wa mkandarasi wa awali ulivunjwa,taratibu za kumpata Mkandarasi mwingine zilifanyika na sasa mkandarasi ameshapatikana na mkataba mpya umesainiwa tayari kwa kuanza utekelezaji wa mradi huu katika hatua iliyobaki. Mradi wa maji katika kijiji cha Muhukuru Lilahi ujenzi wa tanki moja umekamilika.Bomba kuu limelazwa hadi kufikia njia panda ya kwenda kijiji cha Lilahi kwenye geti la Maaskari polisi.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kwa mwaka 2017/2018 Halmashauri inatarajia kutekeleza miradi 7 ya maji katika vijiji vya Mbilo,Mipeta,Magagura,Mbingamhalule,Matomondo,Mpitimbi A,Lipaya,Parangu na Muhukuru Nakawale.Utekelezaji wa miradi hii kwa sasa upo katika hatua ya kutafuta Mtalaamu Mshauri kwa ajili ya upimaji na usanifu wa miradi hii ya maji.Kukamilika kwa miradi hii ya maji 7 kutawezesha idadi ya watu wapatao 33,909 kupata huduma ya maji safi na salama waliopo katika vijiji hivi.

### 3.2 Sekta ya Afya:

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Halmashauri ina Hospitali 1 ya Peramiho inayomilikiwa na Misheni. kituo cha afya kimoja cha Serikali ambacho ni Muhukuru na zahanati 30 kati ya hizo 11 zinamilikiwa na Misheni na 19 zinamilikiwa na Halmashauri. Vituo hivyo vya kutolea huduma vinatoa mgawanyo kiuwiano kama ifuatavyo: -

- Uwiano wa kitanda kwa wagonjwa 1:591
- Uwiano wa kituo cha Afya kwa idadi ya watu 1:50,236
- Uwiano wa Zahanati kwa idadi ya watu 1:5,494

Pamoja na unafuu wa upatikanaji wa huduma za afya katika Halmashauri, bado Halmashauri inaendelea kukabiliwa na magonjwa ya Malaria, HIV/AIDS, kuharisha na magonjwa yanayoenea kwa njia ya hewa . Ugonjwa wa malaria unaongoza kwa asilimia 46 % na kusababisha vifo 90 kati ya wagonjwa wote waliopata huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya ukifuatiwa na magonjwa ya kuharisha .

Kwa upande wa malaria mpango maalumu wa kudhibiti malaria kwa kuhimiza matumizi ya vyandarua vyenye dawa umeanzishwa na umeonyesha mafanikio makubwa kwani wananchi wengi wananunua vyandarua hivyo na kuvitumia. Mpango wa kupambana na maambukizi ya UKIMWI, Halmashauri inaendelea na mkakati uliopo wa kudhibiti kasi ya maambukizi ya UKIMWI ambapo kwa sasa kiwango cha maambukizi ni asilimia 3.9%.

Aidha Halmashauri inaendelea kutoa huduma za afya bure kwa makundi maalum kama vile mama wajawazito, watoto chini ya miaka mitano, walemavu na wazee. Kadhalika idara imeinua kiwango cha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba kwa asilimia 85. Vituo 29 vimefungua Akaunti ya kituo (CHF) kati ya vitu 32. Aidha kaya 6,143 zimejiunga na mfuko wa CHF sawa na asilimia 20% kati ya kaya 30,717. Asilimia 58 ya vituo vya kutolea huduma za afya kunamabango yanaoonyesha; Jina la Kituo, huduma zitolewazo na muda wa kazi pia vituo vyote vina huduma za dirisha la wazee.

#### 3.2.1. Huduma za Kinga:

Huduma za chanjo zimekuwa zikitolewa kwenye vituo vyote vya huduma za afya na kufikia mafanikio ya kuchanja watoto 2,982 sawa na asilimia 94, Pepopunda kwa akina mama wajawazito imefikia asilimia 51 kutoka asilimia 42 ya mwaka 2016.

**3.2.2. Huduma za Lishe:**

Siku za lishe za afya na lishe katika vijiji vyote 56 zilifanyika na kugundua kuwa watoto wa wakiume 4 na wakike 12 wana utapiamlo mkali.. Pia iligundulika kuwa kuna watoto wa kiume 92 na wakike 102 waliodumaa, elimu ya afya ilitolewa ili kuboresha afya kwa watoto hao na kunusuru hali hiyo isitokee tena kwa watoto wengine. Maadhimisho ya Wiki ya unyonyeshaji kwa kata 4 yalifanyika ambapo akina mama 2,500 wajawazito na wanaonyenyesha walihudhuria.

**3.2.3 Huduma za Usafi wa Mazingira:**

Wilaya ina kaya 30,717, kaya 16,680 zimetembelewa sawa na asilima 54 ambapo kaya 10,387 sawa na asilimia 62 zina vyoo bora. Aidha kaya 10,387 zina mashimo ya taka yanayotumika. Kutokana na uhamasishaji wa matumizi ya maji safi na salama kaya 17,816 zinatumia maji safi na salama. Elimu ya Afya bado inaendelea kutolewa ili jamii iendelee kufahamu umuhimu na faida za kutumia maji safi na salama

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri inataraji kutekeleza mikakati ifuatayo ili kuboresha huduma za afya ambayo ni;

1. Kuunda Kamati ya watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi katika ngazi ya Wilaya, kata na vijii vyote.
2. Kufanya mikutno ya kamati hizo kila robo mwaka.
3. Kutembelea kituo cha watoto yatima Chipole na kuwapatia vyakula na sabuni.
4. Kutoa Mafuta maalum ya walemavu wa ngozi (Albino) 52 katika kata zote za Halmashauri yetu.

**3.2 Sekta ya Ujenzi (Barabara):**.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Mtandao wa barabara katika Halmashauri umegawanyika katika makundi manne. Barabara Kuu/Kitaifa, barabara za Mkoa, barabara za Wilaya na barabara za vijijini. Halmashauri ina jumla ya barabara zenye urefu wa kilometa 1070.1 ambazo ni za changarawe na udongo.

**Jedwali 2: BARABARA ZA WILAYA ,AINA NA UREFU (KM)**

| BARABARA | AINA | UREFU (KM) |
|---|---|---|
| Kitaifa/Kuu | Rami | 30 |
| MKOA | Rami | 6 |
| WILAYA | Changarawe | 126.8 |
| | Barabara za udongo | 943.3 |
| **JUMLA** | | **1,106.1** |

Barabara za Halmashauri kwa sababu nyingi ni za changarawe na udongo ziliharibika sana kutokana na mvua nyingi zilizonyesha kwa msimu wa mwaka 2015/2016. Kwa mwaka 2016/2017 Halmashauri ilikarabati barabaraba hizo kwa kuzifanyia matengenezo ya mara kwa mara,matengenezo ya sehemu korofi, matengenezo ya kipindi maalumu, ujenzi na ukarabati wa madaraja.

- Barabara zenye urefu wa Km 128 zilifanyiwa matengenezo ya kawaida ambazo ni barabara za Matomondo-Magagura, Maposeni-Mgazini, Mahiro-Mpingi- Kikunja, Litowa-Mdumduwalo-Maposeni na Shule ya Tanga-Mpandangindo-Parangu
- Barabara zenye urefu wa Km 25 zilifanyiwa matengenezo ya sehemu korofi ambazo ni barabara za Mpitimbi-Ndongosi –Nambendo,Mpandangindo – Liweta,Songea – Mkurumusi –Mpitimbi A.
- Barabara zenye urefu wa Km 18.4 zilifanyiwa matengenezo ya kipindi maalumu ambazo ni barabara za Matomondo- Magagura – Kizuka,Morogoro – Nakahuga,Peramiho – Morogoro – liganga,Muhukuru – Barabarani – Magwamila
- Madaraja 2 yalijengwa katika barabara za Kitulo – Chandarua (Mto Mwombezi),barabara ya Litapwasi – Lyangweni (mto Mwangazi)

**Mheshimiwa mwenyekiti,** Malengo kwa mwaka 2017 /2018 ni kufanya matengenezo ya kawaida Km 75.5, matengenezo ya sehamu korofi Km. 20, matengenezo ya kipindi maalumu Km.26.5 na kujengo daraja moja katika mto Misuku katika barabara ya LMpandangindo- Liweta- Misuku.

### 3.3 Sekta ya Mipango,Takwimu na Ufuatiliaji

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Sekta hii imekuwa ikiratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Kuna mafanikio makubwa ambayo yamejidhihirisha katika ushiriki wa wananchi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia mfumo wa fursa na vikwazo kwa maendeleo (O&OD).

Ushiriki huu unaonekana kupitia programu mbalimbali zinazotekelezwa kama vile Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Fedha za Kujenga Mtaji (CDG), Mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya (DADPs), Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira (RWSSP), Mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu (PFM) na Mpango wa maendeleo ya afya ya msingi (MMAM).

Kwa kutumia Mipango hiyo, miradi mingi ya miundombinu ikiwemo ya ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu, hosteli, maabara,majengo ya utawala, zahanati, nyumba za waganga, miundombinu ya maji na barabara pamoja na uhifadhi wa maliasili na mazingira imetekelezwa kwa mchango wa

fedha na nguvu kazi za wananchi. Kwa ujumla wananchi wametimiza na wanaendelea kutimiza wajibu wao.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,**ufuatiliaji na usimamizi wa miradi mbalimbali ya maendeleo ulifanyika katika mwaka wa fedha 2016/2017.Miradi mbalimbali imetekelezwa ikiwemo miradi ya maji,ujenzi wa madarasa,nyumba za walimu,nyumba za waganga,ofisi za kata na vijiji,majengo ya utawala na mabwalo,majengo ya zahanati na vituo vya afya,ukarabati wa barabara, ujenzi wa madaraja,ukarabati wa skimu za umwagiliaji na ujenzi wa maghala.

Changamoto kubwa iliyopo katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni uwepo wa miradi mingi ya miaka ya nyuma (Viporo). Halmashauri katika mpango na bajeti yake ya mwaka 2017/2018 imezingatia ukamilishaji wa miradi viporo na imetenga fedha kiasi cha Sh.408,118,400 kupitia fedha za ruzuku ya kujenga mtaji (LGCDG) na mapato ya ndani kiasi cha Sh..57,606,560 fedha zitakazotumika katika ukamilishaji wa miradi viporo.

Miradi itakayokamilishwa ni pamoja na ujenzi wa madarasa katika shule mpya za msingi za Lihuhu/Chiulungi,Mbolongo,Ngunguti/Jenista,Muungano, na Njoka,ujenzi wa nyumba za walimu katika shule za msingi mpya za Mhimbasi,Lihuhu, ujenzi wa nymba za waganga katika zahanati za Parangu na Namatuhi. Kukamilisha ujenzi wa sehemu za zahanati za Lipaya na Lugagara ili zianze kutumika,kuendelea na ujenzi wa zahanati za Mpangula,Mdunduwalo na kituo cha afya Ndongosi.Ujenzi wa jengo la utawala katika shule ya sekondari Namihoro na kukamilisha ujenzi wa bwalo la chakula katika sekondari ya Maposeni. Ujenzi wa wodi za wagonjwa katika zahanati za Maposeni na Liula na ujenzi wa ofisi za vijiji vya Makwaya na Matimira B.

### 3.4 Sekta ya Elimu Msingi

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Ufanisi katika sekta za huduma za kijamii ikiwepo elimu upo katika kuboresha maisha ya wananchi (walengwa) moja kwa moja. Kwa kuzingatia hilo Serikali ya awamu ya tano inatoa elimu kuanzia shule ya msingi hadi kidato cha nne bure (Elimu bila malipo). Hii ni kuwapunguzia mzigo mkubwa wananchi na hasa wazazi wenye kipato cha chini katika ulipaji wa ada kwa watoto wao. Kupitia utekelezaji wa sera ya Elimu bila malipo Halmashauri katika sekta ya elimu msingi imetekeleza majukumu yake na kupata mafanikio yafuatayo;

- Kuongezeka kwa kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la awali na darasa la kwanza tofauti na mwaka 2015/1016.

**Jedwali Na. 3 linavyoonyesha kuongezeka kwa uandikishaji kwa darasa la awali na darasa la kwanza**

| MWAKA | DARASA | WALIOTARAJIWA | | | WALIOANDIKISHWA | | | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | ME | KE | JML | ME | KE | JUMLA | |
| 2016 | Awali | 2310 | 2248 | 4558 | 1790 | 1685 | 3475 | 76.24 |
| 2016 | Dalasa 1 | 1800 | 1721 | 3521 | 1528 | 1371 | 1899 | 82.33 |
| 2017 | Awali | 2267 | 2300 | 4567 | 2993 | 2274 | 4667 | 102.2 |
| 2017 | Darasa la 1 | 2080 | 1999 | 4079 | 2555 | 2388 | 4943 | 121.2 |

- Ufaulu wa wanafunzi wa darasa la saba 2016 umeongezeka kwa asilimia 3% ukilinganisha na mwaka 2015. Kiwango cha ufaulu kilikuwa asilimia 72.69, Halmashauri yetu ilishika nafasi ya tatu kati ya Halmashauri 8 zilizopo katika Mkoa wa Ruvuma.
- Mahudhurio ya wanafunzi yameongezaka kufikia asilimia 98
- Miundombinu ya shule na samani zimeboreshwa.
- Utendaji na ari ya kufanya kazi kwa walimu wakuu na waratibu kumeongezeka kutokana na kupewa fedha za madaraka za elimu bila malipo, Jumla ya **Sh 22,004,000** zimetolewa kwa mwaka wa masomo 2016/2017.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**,Halmashauri kwa mwaka 2017/2018 ili kuboresha zaidi kiwango cha elimu imeweka mikakati ifuatayo;

- Kuongeza usajili wa darasa la kwanza na awali kwa asilimia 2% zaidi
- Kuongeza kiwango cha ufaulu wa mtihani wa darasa la saba kufikia asilimia 80%
- Kufanya usimamizi na ufuatiliaji wa taaluma kwenye shule zote 71 zilizopo katika Halmashauri
- Kuboresaha zaidi miundombinu na samani katika shule zetu kupitia fedha za kujenga mtaji LGCDG (Capital development grants-LGCDG)
- Kutoa mafunzo mbalimbali kwa walimu wa masomo na kuboresaha stadi za kujifunza yaani 3k kwa darasa la awali ,darasa la kwanza na darasa la pili.

### 3.5 Sekta ya Elimu Sekondari

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kuna mafanikio makubwa yaliyopatikana katika Halmashauri yetu kupitia sekta hii ya elimu sekondari. Mafanikio haya yametokana na utekelezaji wa sera ya Elimu bila malipo kwa kidato cha kwanza hadi cha nne na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES). Uboreshaji wa miundombinu katika shule za sekondari ulifanyika ikiwemo ukamilishaji wa ujenzi wa nyumba ya mwalimu katika shule ya sekondari Liganga, nyumba ambayo inauwezo wa kuishi familia za walimu 6. Miundombinu ya shule na samani zimeboreshwa kwa ujenzi wa matundu ya vyoo vya walimu na wanafunzi,ukarabati wa madarasa,kukamilisha ujenzi wa maabara,nymba za walimu kupitia fedha za P4R. mafanikio mengine ni haya yafuatayo;

- Kuongezeka kwa kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi wa kidato cha kwanza tofauti na mwaka 2015/1016.
- Mahudhurio ya wanafunzi yameongezaka kufikia asilimia 93

- Samani za maabara zilitolewa na kupelekwa katika shule za sekondari za Mpitimbi,Kilagano na Litapwasi na hivyo kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa masomo ya sayansi.
- Utendaji na ari ya kufanya kazi kwa Wakuu wa Shule uliongezeka kutokana na kupewa fedha za posho ya madaraka za elimu bila malipo, Jumla ya Sh 45,000,000 zilitolewa kwa mwaka wa masomo 2016/2017 kwa wakuu wa shule 15 waliopo.
- Kuongezeka kwa kiwango cha ufaulu kwa mtihani wa kidato cha nne kufikia asilimia 84.6% ambapo kwa mwaka 2015 ilikuwa asilimia 76.12. Halmashauri imekuwa ikishika nafasi ya kwanza Kimkoa kwa miaka mitatu mfululizo na mwaka 2016 Halmashauri ilishika nafasi ya kwanza na kupewa kombe la mshindi wa kwanza
- Kiwango cha ufaulu kwa kidato cha pili kilifikia asilimia 93.3
- Kiwango cha ufaulu kwa kidato cha sita kilikuwa asilimia 100. Hii inamaanisha kwamba hakuna mwanafunzi hata mmoja aliyepata ufaulu wa daraja la 4 wala sifuri.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Mikakati iliyopo ni kuongeza kasi zaidi ya ufuatiliaji na usimamizi wa taalumu katika shule zetu za sekondari ili kufikia lengo lililopo la kushika nafasi ya kwanza Kitaifa katika matokeo ya mtihani wa kidato cha nne na sita. Tunaishukuru Serikali kwa kutupangia na kutuletea walimu wa masomo ya sayansi 9. Walimu walioripoti ni 8 ( Wanaume 4 na Wanawake Ke 4) ambao wamepangiwa kwenda katika shule za sekondari 8 za Maposeni,Darajambili,Liganga,Kilagano,Matimira,Mhalule,Muhukuru na Namatuhi na kila shule imepata mwalimu mmoja.

### 3.6 Sekta ya Maendeleo ya Jamii,Wanawake na Vijana

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Halmashauri inazingatia kutoa huduma kwa kushirikisha jinsia zote wanawake kwa wanaume katika kuhakikisha kuwa fursa na rasilimali zinazopatikana zinawanufaisha watu wote ili kuweza kujikimu kimaisha na hatimaye kupunguza umasikini.
Aidha, Sera ya maendeleo ya jamii ina lengo la kuhakikisha kuwa kwa kila ngazi ya kata kuna mtaalamu wa maendeleo ya jamii, hadi sasa kata 9 zina wataalamu wa maendeleo ya Jamii.
Halmashauri kupitia sekta hii ilitekeleza majukumu mbalimbali kama ifuatavyo;

- Halmashauri ilichangia mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na Vijana kiasi cha Sh 18,000,000 kwa vikundi 17 vyenye wanufaika 128, kati ya hivyo Wanawake vikundi 9 vyenye wanufaika 45 na Vijana vikundi 8 vyenye wanufaika 83.
- Vikundi vyote vya Vijana na Wanawake 17 vilivyopata mikopo vinatoka katika vijiji vya Mgazini, Lusonga, Magagura, Mbingamhalule, Namatuhi, Mhepai, Lyangweni, Mndunduwalo, Peramiho ‘B’, Liganga, Maposeni, Maniamba, Mpangula, Lilahi na Mbingamhalule.
- Ufuatiliaji wa marejesho kwa vikundi vilivyokopeshwa kwa mwaka 2014/2015 na 2015/2016 ulifanyika na jumla ya Tshs 7,490,000 kutoka mfuko wa Vijana na kiasi cha Tshs 13,562,500 kutoka mfuko wa wanawake zilirejeshwa.

- Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika katika Kata ya Mpandangindo kijiji cha Liweta. Shughuli zilizofanyika ni pamoja na utaoaji wa mafunzo ya Ujasiriamali kwa vikundi vya kiuchumi vya akina mama.
- Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika yalifanyika katika kata ya Matimira, kijiji cha Mpingi. Shughuli iliyofanyika ni kuendesha kongamano la watoto.
- Jumla ya vikundi 78 vilisajiliwa na fedha kiasi cha Tshs 2,340,000 zilipatikana.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Halmashauri imeweka kipaumbele cha kutoa fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya kuchangia mifuko ya maendeleo ya vijana na wanawake, ikiwa ni kuendelea kutekeleza sheria ya kutoa asilimia 10 ya makusanyo ya fedha za mapato ya ndani ili kutoa fursa zaidi kwa makundi hayo kupata mikopo na hivyo kukuza uchumi wao. Jumla ya Tshs.138,713,400 zimetengwa katika bajeti ya mwaka 2017/2018.

### 3.6.1 Mapambano dhidi ya UKIMWI/VVU

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Maambukizi ya VVU/UKIMWi katika Halmashauri yetu ni asilimia 3.9%. ikiwa imeshuka toka asilimia 4.6% ya mwaka 2014.Shughuli za mapambano dhidi ya UKIMWI zilifanyika kwa kutumia fedha za bakaa za mwaka 2015/2016. Fedha za bajeti ya mapambano dhidi ya Ukimwi kwa mwaka 2016/2017 hazikupokelewa. Shughuli zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo ;

- Upimaji wa VVU kwa Hiari ulifanyika kwa kufikia vijiji vya Magwamila, Matetereka,Lugagara na Mhepai jumla ya waliopima VVU kwa hiari ni 152 wakiwemo wanaume 70 na wanawake 82 waliokutwa na maambukizi ni 4 mwanaume 1 na wanawake 3.
- Ufuatiliaji na Tathmini ilifanyika kwa vijiji 10 ambavyo ni Matimira, Mpitimbi, Litapwasi , Maposeni, Mgazini, Mhepai,Liweta, Mpandangindo,Muunganozomba na Mipeta.
- Utoaji wa Sare za Shule kwa wanafunzi waliopo katika Mazingira magumu na yatima ulifanyika Jumla ya wanafunzi 116 walipatiwa sare hizo wakiwemo wasichana 57 na vijana 49.
- Mwanafunzi Ahamadi Matola aliweza kusomeshwa kidato cha tano na cha sita, Mtoto huyu ni yatima anatokea katika kijiji cha Muhukuru lilahi na sasa yupo shule ya sekondari Madaba kidato cha sita.
- Mwanafunzi Nestory Milinga kutoka kilagano mwenye ualbino anayesoma kidato cha nne katika Sekondari ya Maposeni aliwezeshwa na Halmashauri na kuweza kufanikisha kununua mahitaji ya Mafuta ya ngozi, Tshirt,Viatu, Tracksut na Kofia.
- Kuwezesha Lishe kwa Mtumishi mmojaa anayeishi na maambukizi ya VVU/UKIMWI
- Upimaji wa VVU kwa hiari Siku ya UKIMWI Duniani ulifanyika kwa kuwafikia wananchi waliopo vijiji vya Mhepai na Maposeni na Jumla ya wanancchi waliopimwa ni 100 wakiwemo wanaume 49 na wanawake 51 waliokutwa na maambukizi ni wanaume 2 na mwanamke 1.

- Kikao 1 cha wadau wa Mapambano dhidi ya UKIMWI,kilifanyika Wadau 15 walihudhuria na kila mmoja alitoa taarifa zake za kazi na maeneo anayofanyia kazi sambamba na mipango kazi yao.
- Kujenga uwezo kwa kamati za kudhibiti UKIMWI za vijiji,shughuli za kujenga uwezo zilifanyika katika kamati za vijiji vya Kilagano, Mhepai,Mgazini, Lugagara na Muungano zomba.
- Uwezeshaji wa miradi kwa makundi tete ulifanyika, Makundi 3 yameweza kuwezeshwa miradi ya Nguruwe ili yaweze kujikomboa kiuchumi makundi hayo ni kutoka katika vijiji vya Maposeni, Litapwasi na Mpitimbi A yenye jumla ya wanachama 67 wakiwemo wanaume 31 na wanawake 36.
- Clubs za vijana zimeundwa mashuleni ikiwa ni utoaji wa elimu ya UKIMWI katika shule za sekondari za Mpitimbi, Muhukuru lilahi, Maposeni ,Ndongosi na Namatuhi

**Mheshimiwa mwenyekiti**, Mikakati ya mapambano dhidi ya maambukizi ya UKIMWI/VVU itaongezwa zaidi katika mwaka 2017/2018 ili kuweza kutoa elimu zaidi kwa wananchi na hivyo kuzuia kuendelea kuongezeka kwa maambukizi mapya.

### 3.7 Sekta ya Kilimo:

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Uchumi wa Halmashauri hutegemea zaidi kilimo. Wakazi karibu wote wa Halmashauri yetu hupata riziki zao kutokana na shughuli za kilimo. Aidha asilimia 80% ya mapato yote ya ndani katika Halmashauri hutoka katika sekta hii,sekta nyingine zilizosalia zinachangia chini ya asilimia 20%. Tafsiri ya takwimu hizi ni kuwa upanuzi, uboreshaji na uendelezaji wa shughuli za kilimo ndiyo njia inayoweza kukuza uchumi na kuondoa umasikini katika Halmashauri yetu.

#### 3.7.1 Utekelezaji wa malengo ya mazao ya chakula na biashara msimu 2016/2017

Katika msimu wa **2016/17**, Halmashauri ilikadiria wakulima walime jumla ya hekta **103,307** za mazao ya chakula na biashara zitakazozalisha jumla ya tani 299,565.8. Utekelezaji zililimwa Hekta 100,824 na kutoa tani **288,400** za mazao ya chakula na biashara .

Aidha, hekta **5,463** za mazao ya mbogamboga na matunda zitakazozalisha jumla ya tani **109,265** na hivyo basi tunategemea kupata ziada ya tani **223,728.2 za mazao ya chakula** baada ya kutoa tani **56,570.8** za chakula kwa idadi ya watu **141,427.** na mahindi ziada ni tani **113,840.2** ambazo tani **700** hadi **800** zinategemewa kununuliwa na kitengo cha taifa cha hifadhi ya chakula (NFRA) na tani **113,040.2** zilizobaki zitanunuliwa na makampuni Binafsa na wafanyabiashara binafsi.

### 3.7.2 Kilimo cha Kiangazi.

Kutakuwa na mavuno ya mazao ya kilimo cha umwagiliaji ambacho kinatarajiwa kitoe tani **6,966.3** kutoka kwenye hekta **4,975.5.** Mchanganuo wa kilimo cha msimu wa kilimo **2016/2017** na malengo ya Kilimo kwa Msimu **2017/2018** ni kama unavyonyesha kwenye majedwali hapo chini;.

**Jedwali Na.2 linaonyesha malengo ya kilimo mazao ya chakula msimu 2016/2017:**

| Na | ZAO | 2016/2017 | |
|---|---|---|---|
| | | **Lengo (Hekta)** | **Matarajio. (Tani)** |
| 1 | Mahindi | 55174.5 | 187592.9 |
| 2 | Mpunga | 11666.4 | 36165.8 |
| 3 | Mihogo | 12082.6 | 26944.2 |
| 4 | Maharage | 5655.2 | 5938.0 |
| 5 | Ulezi | 2885.6 | 1587.1 |
| 6 | Viazi Vitamu | 2588.8 | 19416.0 |
| 7 | Ndizi | 743.4 | 13381.2 |
| 8 | Mbaazi | 530.0 | 280.9 |
| | **JUMLA** | **91326.5** | **291306.1** |

**Jedwali Na. 3 linaonyesha malengo ya kilimo kwa mazao ya biashara msimu 2016/2017**

| Na | ZAO | 2016/2017 | |
|---|---|---|---|
| | | **Lengo (Hekta)** | **Matarajio. (Tani)** |
| 1 | Kahawa | 1858.6 | 892.4 |
| 2 | Korosho | 154.2 | 18.0 |
| 3 | Tumbaku | 385.5 | 312.3 |
| 4 | Ufuta | 2373 | 1898.4 |
| 5 | Alizeti | 2519.2 | 2015.4 |
| 6 | Karanga | 1221.2 | 732.7 |
| 7 | Soya | 3451.6 | 2243.5 |
| 8 | Tangawizi | **15** | 147.0 |
| | **JUMLA** | **11,978.3** | **8,259.7** |

**Jedwali Na. 4 Utekelezaji wa malengo ya kilimo msimu 2016/2017 Mazao ya chakula:**

| MALENGO | | | | UTEKELEZAJI | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Na.** | **ZAO** | **HA** | **TANI** | **HA** | **(Matarajio) TANI** |
| 1. | Mahindi | 55,175 | 187,592.9 | 54,072 | 183,845 |
| 2. | Mpunga | 11,666 | 36165.8 | 11,316 | 29,422 |
| 3. | Muhogo | 12,084 | 26,944.2 | 11,842 | *27237* |
| 4. | Maharagwe | 5,655 | 5,938.0 | 5,542 | 5,819 |
| 5. | Ulezi | 2,886 | 1,587.1 | 2828 | 1,555 |
| 6. | V/vitamu | 2,589 | 19,416.0 | 2537 | *19028* |
| 7. | Ndizi | 743 | 13,381.2 | 728 | 13104 |
| 8. | Mbaazi | 530 | 280.9 | 535 | 289 |
| **JUMLA NDOGO** | | **91,328** | **291,306.1** | **89,400** | **280,299** |

**Jedwali Na. 5 Utekelezaji wa malengo ya kilimo msimu 2016/2017 Mazao ya Biashara**

| MALENGO | | | | UTEKELEZAJI | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Na.** | **ZAO** | **HA** | **TANI** | **HA** | **TANI** |
| 1. | Kahawa | 1,859 | 892.4 | 1821 | 1,200 |
| 2. | Korosho | 154 | 18.0 | 151 | 17 |
| 3. | Tumbaku | 386 | 312.3 | 18 | 8 |
| 4. | Ufuta | 2,373 | 1,898.4 | 2326 | 1396 |
| 5. | Alizeti | 2,519 | 2015.4 | 2468 | 1975 |
| 6. | Karanga | 1,221 | 732.7 | 1197 | 718 |
| 7. | Soya | 3,452 | 2,243.5 | 3383 | 2199 |
| 8. | Tangawizi | 15 | 147.0 | 60 | 588 |
| | **JUMLA NDOGO** | **11,979** | **8,259.7** | **11,424** | **8,101** |
| | **JUMLA** | **103,307** | **299,565.8** | **100,824** | **288,400** |

**Jedwali Na. 6 Malengo ya kilimo msimu 2017/2018**

| ZAO | 2017/2018 | |
|---|---|---|
| | **Lengo(Ha)** | **Matarajio ya uzalishaji (Tani)** |
| **Mazao ya Chakula** | | |
| Mahindi | 56,830 | 204,588 |
| Mpunga | 11,993 | 38,378 |
| Ulezi | 2,961 | 1,717 |
| Mihogo | 12,385 | 27,866 |
| Viazi Vitamu | 2,656 | 19,920 |
| Ndizi | 762 | 13,716 |
| Mbaazi | 544 | 299 |
| Maharage | 5,802 | 6,150 |
| **JUMLA NDOGO** | **93,933** | **312,634** |
| **MAZAO YA BIASHARA** | | |
| Soya | 3,518 | 2,462 |
| Ufuta | 2,304 | 1,613 |
| Alizeti | 2,529 | 2,023 |
| Karanga | 2,064 | 1,238 |
| Tumbaku | 394 | 323 |
| Kahawa | 1,887 | 1,510 |
| Korosho | 124 | 13 |
| Tangawizi | 100 | 980 |
| **JUMLA NDOGO** | **12,920** | **10,162** |
| **JUMLA KUU** | **106,853** | **322,796** |

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kutokana na majedwali hapo juu yanayoonyesha malengo na utekelezaji wa msimu wa kilimo kwa mwaka 2016/2017 kwa mazao ya chakula, Halmashauri yetu haitakuwa na njaa kwa mwaka huu 2017. Mazao ya chakula yamezalilishwa ya kutosha kwa matumizi ya chakula na inabaki ziada ambayo inaweza kuuzwa katika maeneo mengine ya nchi yetu.

Shughuli zingine zilizofanyika ni;

- Kusimamia na kufuatilia ujenzi wa soko la kimataifa na kituo cha kuongeza thamani ya mazao katika kituo cha OTC Lilambo, Ujenzi wa soko unaendelea, Ujenzi wa Jengo la Kituo cha Usindikaji umekamilika na hatua iliyopo ni ya mchakato wa manunuzi ya mashine ya usindikaji ambapo tathmini ya zabuni imefanyika na kupelekwa Makao Makuu ya Program ya MIVARF Arusha.
- Shughuli ya Kusajili upya vikundi vya umwagiliaji vya Skimu kumi (10) za Muhukuru Lilahi, Namatuhi, Njoka, Mptimbi (B), Mptimbi (A), Ndongosi, Litisha, Morogoro, Nakahuga na Parangu ilifanyika. Hii ni utekelezaji wa agizo la Serikali la kuzitaka skimu zote za umwagiliaji kusajiliwa upya na kuwa na katiba zinazofanana kwa kila skimu. Zoezi la usajili bado linaendelea na skimu ambazo bado hazijisaliwa ni nne (4) ambazo ni Litapwasi, Matimila, Nambendo na Magima
- Ukarabati wa eneo la mfereji mkuu lililoharibiwa na mvua za masika katika skim ya Njoka, Namatuhi. Ulifanyika. Kikundi kiligharamia trip mbili za mawe, trip tatu za kifusi, trip mbili za mchanga na mifuko 20 ya saruji kupitia mfuko wao wa uchakavu. Halmashauri ilichangia gari na mafuta lita 65 kwa ajili ya kuwasogezea vifaa hivyo

Aidha mikakati ya Halmashauri kwa mwaka 2017/2018 ya kuendeleza kilimo cha mazao ya chakula na biashara ni;

- Kuwepo kwa daftari la utendaji kazi za huduma za ugani katika kata na vijiji
- Ununuzi wa pikipiki 4 kwa ajili ya maafisa ugani
- Ununuzi wa video kamera na projekta
- Kutoa mafunzo rejea kwa maafisa ugani 35 ndani na nje ya Halmashauri na wakulima 500 kwa kufanya ziara za mafunzo
- Kuwezesha ujenzi wa nyumba moja ya mtumishi katika kijiji cha Litapwasi
- Kuweka thamani katika kituo cha Kilimo OTC Lilambo

### 3.7.3 Mbolea:

**Mheshimiwa Mwenyekiti**,.Uhakiki wa usambazaji wa pembejeo za kilimo za ruzuku ulifanyika kwa kushirikiana na Mkaguzi wa Ndani ambapo jumla ya seti 11,000 zilizogawiwa kwa Halmasahuri zilihakikiwa. Hili lilikuwa ni agizo la Serikali kwa lengo la kuandaa malipo ya mawakala waliosambaza pembejeo kwa msimu wa kilimo 2015/16

.

Kwa mwaka 2016/2017 Halmashauri ilipokea mbegu za mahindi tani 93.6 zilizowanufaisha wakulima 9,360, Mbolea ya kupandia tani 481.5 na Mbolea ya kukuzia tani 481.5 zilizowanufaisha wakulima 9,630 ikiwa ni ruzuku ya pembejeo kutoka Serikalini.Pembejeo zote hizi ziligawiwa kwa wananchi.

### 3.8 Sekta ya Mifugo na Uvuvi

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Halmashauri ya Wilaya Songea ina jumla ya ng'ombe 13,123, mbuzi 37,089, nguruwe 17,159 kuku 125,908 kati ya hao kuku wa kienyeji ni 117,609 na wa kisasa ni 4,299, bata 3,618,punda 126,mbwa 2,918, paka 194 na sungura 196. Jitihada zinaendelea kufanywa ili kuongeza mifugo na mazao yake kwa kushirikiana na wahisani hasa "Heifer Project International" kupitia CARITAS na Mfuko wa ushirikiano wa Tanzania na Japani (Tanzania Food Aid Counterpart Fund.

#### 3.8.1 Miundo mbinu ya mifugo

- Idadi ya majosho yote katika Halmashauri ni 6, yanayofanya kazi ni 3, yasiyofanya kazi ni 3. Pia kuna josho la kupuliza (Spray race) 1 ambalo linafanya kazi.
- Halmashauri ina machinjio ya kati (Mini abattoirs) 1 katika kata ya Magagura ambayo inafanya kazi kwa sasa.
- Halmashauri inaendelea kukamilisha ujenzi wa Mnada wa awali wa Mifugo (Livestock Primary Market) katika kijiji cha Mhepai kwa kujenga choo na uzio.

### 3.9 Sekta ya Maliasili:

Mheshimiwa Mwenyekiti,Sekta ya Maliasili inahusika na sekta ndogo za misitu, nyuki, wanyamapori na Utalii. Pia inajihusisha na usimamizi wa rasilimali za Maliasili na kuhakikisha matumizi endelevu ya maliasili hizo kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo. Halmashauri ina misitu ya hifadhi 9. Kati ya misitu hiyo 6 ni ya Serikali Kuu ambayo ni Msitu wa nishati Songea, Chabruma, Machinjioni, na East-West Matogoro. Misitu ya hifadhi inayomilikiwa na Halmashauri ni 2 nayo ni Maposeni, na Lihanje. Shughuli za uwindaji zitaendelea kupewa kipaumbele kwa kuanzisha vitalu zaidi.Hata hivyo shughuli za utalii hazijaendelezwa sana kutokana na ukosefu wa uwekezaji katika sekta hii.

Lengo la upandaji miti katika mwaka 2017/2018 ilikuwa ni kupanda miti 1,500,000. Lengo hili litafikiwa kwa kuotesha miti na kuipanda, sambamba na upandaji wa miti ya maotea, Vigingi (Cuttings) na mbegu.

### 3.10 Sekta ya Ushirika:

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Halmashauri inaipa umuhimu mkubwa sana sekta hii kutokana na mchango wake katika mpango wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Wilaya ina jumla ya vyama vya ushirika vya mazao 8, chama kikuu cha ushirika kimoja, vyama vya akiba na mikopo vya Kata vipo 12 . SACCOS za Kata zina jumla ya wanachama 11,188 Hisa za wananchama ni Shs. 127,215,400 akiba/amana jumla shs.707,816,084 Hadi sasa SACCOS za Kata zimeweza kutoa mikopo yenye jumla ya Shs. 1,455,237,641

Pamoja na SACCOS za Kata, Halmashauri ina SACCOS 3 ngazi ya wilaya zikiwa za Wafanyakazi. Pia kuna SACCOs 3 za makundi maalumu.. SACCOS hizo zina jumla ya Wanachama 2368, hisa za shilingi 95,037,019 na akiba/amana ya shilingi 252,240,728 mikopo iliyotolewa kwa mwaka 2011 ni jumla ya shilingi 1,660,625,000.

Tatizo kubwa la vyama vya ushirika ni ukosefu wa mbinu za ushindani wa masoko katika mfumo wa hivi sasa wa soko huria. Halmashauri inaendelea na mkakati wa kuanzisha taasisi za benki vijijini (Rural Financial Institutions /MIVARF) ili wananchi waweze kufikiwa na vyanzo vya fedha kwa ajili ya shughuli zao za kiuchumi.

Kipaumbele cha sekta hii katika mwaka wa fedha 2017/2018 ni kuongeza amana/akiba, wanachama na kuunganisha SACCOs

### 3.11 Sekta ya Ardhi:

Mheshimiwa mwenyekiti, Sekta hii inajihusisha zaidi na upimaji wa viwanja, mashamba na uendelezaji wa makazi. Kero kubwa katika sekta hii ni malalamiko ya migogoro inayotokana na mipaka ya vijiji, migogoro ya mashamba na viwanja.Katika mwaka wa fedha 2016/2017 sekta hii imetekeleza shughuli zifuatazo;

- Kukusanya kodi ya Ardhi kiasi cha Tsh 39,740,558.55 na kuweza kutuma Wizarani Matarajio yalikuwa kukusanya Sh. 50,000,000/=.
- Viwanja 110 vilikaguliwa katika mji mdogo wa Peramiho kati ya viwanja 100 vilivyotarajiwa ikiwa ni sawa na mafanikio ya asilimia 110.
- Alama za viwanja 150 zilionyeshwa katika mji mdogo wa Peramiho kati ya viwanja 155 vilivyotarajiwa...
- Taarifa za viwanja 980 vya Peramiho A na B pamoja na viwanja 620 vya Mkenda ziliingizwa katika mfumo wa kielekroniki.
- Viwanja vipatavyo 122 kati ya viwanja 150 vilivyotarajiwa kupimwa kwenye eneo la mji mdogo Mkenda viwanja 102 na Peramiho viwanja 20 vilipimwa . Eneo lililofikiwa kwa upande wa Peramiho ni eneo la Njunde, Namihoro na Mnyonga.
- Jumla ya wananchi 18 walipimiwa maeneo ya mashamba yao yaliyokuwa na ukubwa wa ekari 586.83 walioomba huduma ya kupimiwa mashamba yao.
- Uthamini wa mali za Halmashauri zinazohamishika na zisizohamishika kama vile Ardhi, majengo, mashine, samani, nk.ulifanyika, Thamani ya mali za Halmashauri kwa ujumla wake ni Tsh. 44,232,000,000/=

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Matarajio ni kuwa Halmashauri itaendelea na mikakati yake ya kuhakikisha kuwa Sheria ya Ardhi namba 5 ya Vijiji ya mwaka 1999 inaelimishwa kwa wananchi.Pia Halmashauri itaendelea na kuandaa matumizi bora ya ardhi katika vijiji kama njia ya kupunguza migogoro ya mipaka na mashamba na hasa migogoro inayotokana na uvamizi wa wafugaji na kuwamilikisha hati miliki wananchi pamoja na hati miliki za kimila.

### 3.12 Sekta ya Biashara:

Biashara katika Halmashauri kwa sehemu kubwa inaendeshwa na watu binafsi na makampuni ya kununua mazao ya biashara hasa tumbaku na mahindi. Kwa mwaka 2016/2017 hali ya biashara kwa mazao hayo ya Tumbaku na Mahindi ilikuwa ya kuridhisha hasa baada ya Kitengo cha Taifa cha Hifadhi ya Chakula kununua mahindi yote yaliyokusudiwa kuuzwa. Aidha zao la tumbaku halikupata bei nzuri inayolingana na gharama za

uzalishaji. Juhudi zinaendelea kufanyika katika kuboresha huduma ya masoko ili kuwapa fursa wananchi kupata bei nzuri ya mazao.

**3.0 UTAWALA BORA:**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Halmashauri ya Wilaya Songea imekuwa ikitekeleza shughuli zote kwa kuzingatia dhana ya utawala bora. Vikao vyote vya kisheria katika ngazi zote vimekuwa vikifanyika. Aidha suala la uwazi katika mapokezi ya fedha na matumizi yake limefanyika kwa kiwango cha hali ya juu kwa mfano kuwapa taarifa Waheshimiwa Madiwani,Maafisa watendaji wa kata na vijiji na kwa kubandika katika mbao zote za matangazo. Wananchi walishirikishwa kikamilifu katika kupanga, kutekeleza na kutathimini miradi yao ya maendeleo..

Aidha suala la Rushwa na maadili ya watumishi na Madiwani yalizingatiwa katika mwaka huu 2016/2017. Hapakuwepo na tuhuma za watumishi au Waheshimiwa Madiwani kupokea rushwa au kuvunja maadili ya kazi zao,hivyo kuifanya Kamati ya maadili kutokuwa na kesi za kujadili.

**6.0 CHANGAMOTO KWA MWAKA 2016/2017**

1. Miradi mingi haikutekelezwa kutokana na fedha nyingi kutofika kabisa au kutofika kwa wakati toka Serikali kuu (HAZINA)
2. Mchango hafifu wa nguvu za wananchi katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo maandalizi ya vifaa kama tofari,mchanga na mawe .
3. Ufinyu wa ukomo wa bajeti uliotolewa na Serikali kwa fedha za miradi ya maendeleo .Hali hii ilipelekea miradi mingi iliyoibuliwa na wananchi kutoingizwa katika mpango na bajeti ya mwaka 2016/2017 au kuingizwa na kukasimiwa kiasi cha fedha kisichokidhi mahitaji.
4. Mfumuko wa bei wa vifaa vya viwandani na uzalishaji ulisababisha gharama kuwa kubwa na kusababisha kutokamilika kwa baadhi ya miradi kama ilivyopangwa.
5. Kuwepo kwa miradi mingi ya miaka ya nyuma (Viporo) isiyokamilika.

**7.0 HATUA ZILIZOCHUKULIWA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO HIZO**

1. Halmashauri ilikuwa ikifanya mawasiliano/kufuatilia mara kwa mara HAZINA ili kutia msukumo wa kutolewa kwa fedha za utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo
2. Wananchi waliendelea kuhamasishwa na kushirikishwa ili waongeze juhudi za kuchangia nguvu zao katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo ni wao wenyewe waliiibua kupitia mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (O &OD)
3. Halmashauri iliongeza juhudi katika kukusanya mapato yake ya ndani ili kuweza kupata fedha zaidi za kusaidia utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kidogo.Pia iliendelea kuwahamasisha wadau wengine wa maendeleo yakiwemo Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGOs),Mashirika ya kijamii (CBOs),Mashirika ya kidini (FBOs),Taasisi na Sekta binafsi kwa ujumla ili ziweze kusaidia katika utekelezaji wa miradi/shughuli mbalimbali za maendeleo kwa Halmashauri yetu.

4. Halmashauri katika mpango na bajeti yake ya mwaka 2017/2018 imetenga fedha kwa ajili ya kukamilisha miradi viporo kupitia fedha za ruzuku ya Serikali za mitaa (LGCDG) na fedha zinazotokana na makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri (Own source).

**8.0 Hitimisho**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, yaliyopangwa na kutekelezwa na Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2016/2017 yalikuwa mengi sana,kiasi kwamba hayawezi kuonekana au kutajwa yote katika taarifa hii. Kwa kuhitimisha Halmashauri katika mwaka wa fedha 2017/2018 imejipanga kutekeleza mikakati yote iliyojiwekea katika Mpango na Bajeti yake ikiwemo ya kuongeza ukusanyaji wa mapato yake ya ndani,kutekeleza miradi kwa wakati,kutekeleza Ilani ya uchaguzi mkuu ya CCM ya mwaka 2015,Malengo ya Maendeleo endelevu (SDG),kutekeleza kauli mbiu ya Serikali ya awamu ya tano ya Viwanda na kuendelea kutekeleza shughuli zake kwa kufuata Sheria,Kanuni,taratibu na miongozo mbalimbali inayotolewa na Serikali.

Dhana ya ushirikishwaji wa wananchi na jamii itaendelea kudumishwa na hasa katika suala zima la utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili wananchi wajenge imani na kushiriki zaidi ikiwa ni pamoja na kuiona miradi kuwa ni mali yao na inatekelezwa kwa manufaa yao.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Naomba kuwasilisha



**Simon M.M. Bulenganija**
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**SONGEA**